HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 08 Januari - Aprili 2011

# Haki na Usawa katika Milki ya Ardhi viwe nguzo muhimu ya Katiba Mpya

Na. Cathbert Tomitho

Katiba ni sheria mama katika nchi yoyote. Ni sheria mama kutokana na ukweli kuwa sheria zote zinazotungwa zinatakiwa ziwe na msingi wake katika Katiba. Lakini pia, Katiba ni chombo muhimu katika maisha ya nchi na wananchi wake kwa kuwa inaainisha masuala yote yanayohusu utendaji na uhusiano wa kimamlaka kati ya mihimili mikuu ya dola yaani Bunge, Serikali na Mahakama na masuala mengine muhimu kama vile uchaguzi, mfumo wa kisiasa na mahusiano ya kimataifa.

Katiba ya Tanzania ina historia ndefu kutokana na ukweli kuwa imepitia katika vipindi mbalimbali kuanzia nyakati za ukoloni na baada ya kupata uhuru mwaka 1961. Katiba inayotumika sasa ni ya mwaka 1977 lakini imeshafanyiwa marekebisho mara kumi na nne tangu ilipotungwa. Hata hivyo, kumekuwa na mijadala ya muda mrefu katika jamii ikidai kutungwa kwa Katiba mpya kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni pamoja na kutaka kuwe na ushiriki Endelea Uk.3



Prof. Issa Shivji akitoa mada kwenye Kongamano la Kitaifa juu ya umuhimu wa kuifanya ardhi kuwa nguzo muhimu ya Katiba lililofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Februari 2011.

## NUKUU YA TOLEO

Kwa vile fursa ya kujadili na kuandika Katiba mpya imejitokeza, na tuichukue hii kuwa pia fursa ya kufanya mabadiliko ya kimfumo katika ugawaji na usimamizi wa ardhi ili kutoa ulinzi stahiki wa haki za wananchi juu ya rasilimali hii muhimu na kukidhi matakwa na maslahi ya watumiaji wa ardhi ambao ndio hao wanaodai mabadiliko, maana wao ndio hukumbana na adha ya migogoro inayowapotezea uhai na mali zao.

*Yefred Myenzi*

## YALIYOMO


- Tahariri Uk.2
- Umuhimu wa Ardhi na Ulinzi Uk.3-5
- Mjadala wa Katiba: Uzoefu kutoka Kenya. 4
- Katiba bora itatokana na Ushiriki 6 -7
- Wajibu wa NGOs Uk. 8 - 9
- Mawazo ya Wananchi Uk. 10
- Kona ya Ufahamu Uk. 11
- Machapisho Uk. 12

**ARDHI NI UHAI ni jarida la *Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa* Haki za Ardhi (HAKIARDHI), ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.**

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Mhariri**
Yefred E. Myenzi

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe
Alice Shamge - Mjumbe

**Mchapishaji**
Hakiardhi

## UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI

WASOMAJI wa jarida hili mnakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, ushauri, maoni au kwa kuandika makala. (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani zifuatazo:

Mhariri:
**ARDHI NI UHAI**
**S.L.P 75885**
**Dar es Salaam**

Email:
**info@hakiardhi.org**

**Mchapaji**
Ecoprint Ltd.

Email:
**ecoprinttz@yahoo.com**

# TAHARIRI

## Katiba Mpya itoe ulinzi zaidi kwa Rasilimali za Taifa

Ardhi kwa jamii nyingi za Kiafrika ni nguzo muhimu pengine kuliko nyingine yoyote katika maisha yao. Ukiacha imani za kidini hasa ile ya wakristo wanaoamini kuwa chimbuko la mwanadamu ni uumbaji uliofanywa na Mungu kwa kufinyanga udongo na kupulizia pumzi ya uhai, ardhi ndiyo rasilimali pekee inayoendeleza uhai wa mwanadamu na viumbe vingine kwa kuvipa chakula, maji, maliasili kama mimea na misitu yenye umuhimu wa kipekee kwa dawa za binadamu na mifugo yake, wanyamapori, na, ndicho chanzo cha maendeleo ya kila namna kwa binadamu. Kutokana na umuhimu huo wa ardhi, ni sharti mifumo na mipango ya ugawaji, usimamizi na matumzi yake ikidhi matakwa na maslahi ya kila kundi katika jamii ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima na kuwezesha maisha endelevu kwa kila mwananchi anayetegemea ardhi.

Kwa kutambua umuhimu wa kuwepo kwa mifumo na mipango ya aina hiyo, kumekuwa na madai ya muda mrefu kutoka kwenye jamii na hasa makundi ya wanaharakati wa masuala ya haki za ardhi na haki za binadamu kuwa mfumo wa milki ya ardhi ya Tanzania ubadilike kwa kufanya mambo matatu ya msingi. Kwanza, kuboresha muundo wa ugawaji na usimamizi wa ardhi kwa kupunguza mamlaka ya kiutendaji na kiusimamizi yaliyolimbikizwa kwenye vyombo vya serikali kuu na kuyapeleka katika vyombo vya serikali za mitaa hususan vile vyenye uwakilishi wa wananchi kama vile Mkutano Mkuu wa Kijiji. Pili, kuvitambua vyombo hivyo vya kiusimamizi wa ardhi ya wananchi hasa Mkutano Mkuu wa Kijiji kuwa chombo cha kikatiba na tatu, kuingiza katika Katiba ya nchi, haki ya kila raia kumiliki ardhi ikiwa ni pamoja na kuingiza mfumo wa milki na usimamizi wake kama nguzo muhimu za Katiba. Mabadiliko haya kwa pamoja, yamekuwa yakielezwa kuwa yataongeza sio tu uhakika wa milki ya ardhi kwa wananchi bali pia yataepusha migogoro katika matumizi ya ardhi baina ya makundi mbalimbali ya kijamii ambayo imekuwa ikishuhudiwa kila uchao. La muhimu kuliko yote, uingizwaji wa mfumo wa ardhi kwenye Katiba utatoa fursa kubwa kwa wananchi kushiriki katika marekebisho ya mfumo huo pale itakapotokea haja ya kufanya hivyo kwani mabadiliko yoyote ya Katiba sharti yashirikishe wananchi kikamilifu.

Katika toleo hili maalumu la jarida letu la Ardhi ni Uhai, tunajaribu kuendeleza mjadala ulioibuliwa na washiriki wa kongamano la kitaifa juu ya umuhimu wa kuifanya ardhi kuwa nguzo muhimu ya Katiba, ambalo lilifanyika mwezi Februari 2011 jijini Dar es salaam na kushirikisha wanaharakati wa masuala ya ardhi kutoka Kenya na Uganda. Pamoja na kutoa mapendekezo kadha wa kadha ya namna ya kupata Katiba yenye uhalali kwa wananchi, washiriki hao takribani 130 toka sehemu mbalimbali nchini, waliainisha michakato mbalimbali inayoweza kusaidia kuipa ulinzi wa kikatiba rasilimali ardhi kwa minajili ya kuendeleza ustawi wa maisha ya watanzania hususan wazalishaji wadogo wadogo wanaotegemea ardhi. Kwa vile fursa ya kujadili na kuandika Katiba mpya imejitokeza, na tuichukue hii kuwa pia fursa ya kufanya mabadiliko ya kimfumo katika ugawaji na usimamizi wa ardhi ili kutoa ulinzi stahiki wa haki za wananchi juu ya rasilimali hii muhimu na kukidhi matakwa na maslahi ya watumiaji wa ardhi ambao ndio hao wanaodai mabadiliko, maana wao ndio hukumbana na adha ya migogoro inayowapotezea uhai na mali zao. Kamwe tusiipoteze fursa hii adhimu.

# Haki na Usawa katika Milki ya Ardhi...

Inatoka uk. 1

mpana zaidi wa wananchi katika masuala mbalimbali yanayowahusu na kuingizwa kwa mambo ambayo hayakuzingatiwa katika mabadiliko yaliyofanywa mara zote hizo kumi na nne. Moja ya mambo hayo ni umuhimu wa kuzitambua na kuzilinda rasilimali za taifa kama vile ardhi, madini, misitu na nyinginezo kwa maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla. Kwa hali ilivyo sasa, Katiba inatoa kauli ya ujumla tu kuwa kila mtu ana haki ya kumiliki mali na kupata ulinzi wa mali hiyo lakini haitamkwi moja kwa moja ni mali au rasilimali zipi na kwa mfumo gani.

Kwa kutambua umuhimu wa hoja hizi kupewa fursa ya kujadiliwa kwa kina, HAKIARDHI iliandaa Kongamano la Kitaifa la masuala ya ardhi ambalo mada kuu ilikuwa ni "Uhakika wa ardhi na rasilimali za taifa kama nguzo muhimu katika katiba mpya."ili wananchi wa kada mbalimbali washiriki katika kujadiliana na kutoa mawazo yao kuhusiana na namna bora zaidi ya kuimarisha ulinzi wa rasilimali ardhi na uhakika wa milki na matumizi yake kwa wananchi wa Tanzania. Kongamano hili lililofanyika mwezi Februari 2011 katika ukumbi wa Hoteli ya Landmark iliyoko Ubungo jijini Dar es salaam, lilihudhuriwa na washiriki takribani 130 kutoka sehemu mbalimbali nchini Tanzania.

# Umuhimu wa Ardhi na Ulinzi wa Rasilimali katika Katiba

Akiwasilisha mada ya ufunguzi juu ya "Umuhimu wa ardhi na ulinzi wa rasilimali katika katiba." Profesa Issa Shivji ambaye ni mmoja wa waanzilishi wa HAKIARDHI na mjumbe wa Baraza la Ushauri la shirika hili, alisema kuwa suala la rasilimali za nchi kupewa ulinzi wa kikatiba ni muhimu kama ilivyo kwa masuala ya kimadaraka kama vile tume ya uchaguzi, mamlaka ya watendaji mbalimbali wa serikali, masuala ya uraia, itikadi ya nchi na mfumo wa siasa katika kipindi hiki cha mageuzi. Umuhimu wa suala la rasilimali kupewa ulinzi wa kikatiba unatokana na ukweli kuwa; Katiba ni kielelezo cha maandishi cha muafaka wa wananchi na si mkataba baina ya wananchi na viongozi wao kama ambavyo wanasiasa wengi wamekuwa wakisema. Kwa maana nyingine, Katiba ni mali ya wananchi na sio zawadi kutoka kwa watawala wao na ndio maana wananchi wanatakiwa kuwa kiini cha michakato ya upatikanaji wa Katiba na yanayopaswa kuwa ndani yake, na hapo ndipo Katiba hupata uhalali hasa umiliki wa wananchi kwa kuwa inakuwa ni zao lao ikilinda matakwa na maslahi yao. Na hapa ieleweke kwamba hakuna maslahi makubwa kuliko ardhi ambayo ndiyo msingi wa maisha na maendeleo yao.

Kwa mujibu wa Prof. Shivji, madai ya ardhi kuingizwa kwenye Katiba si mapya, kwani, yalitolewa na wananchi tangu mapema miaka ya tisini kupitia Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Masuala ya Ardhi ambayo iliwasilisha suala hilo kama sehemu ya mapendekezo ya kimfumo lakini halikuzingatiwa katika sheria mpya za 1999 japo lilitajwa tu katika sera bila watawala kujua linamaanisha nini. Akifafanua zaidi, shivji anasema, "ardhi kwa wananchi

Endelea Uk.5



*Uwekezaji mkubwa kama huu katika sekta ya Madini - Je, unawasaidia wananchi waishio jirani?*



# Mjadala wa Katiba usiwekewe mipaka wala vikwazo katika uhuru wa mawazo: Uzoefu kutoka Kenya



Na Lilian Mkusa

Na Odenda Lumumba

Ni kazi ngumu lakini hatimaye tuliiweza kwa vile tulidhamiria, na wala hatukukata tamaa wala kukubali kukatishwa tamaa na kitu wala mtu yoyote" Ni kauli yenye nguvu na hamasa kubwa anayoanza nayo mtoa mada juu ya uzoefu wa Kenya katika kuandika Katiba mpya iliyojumuisha kikamilifu masuala ya ardhi na rasilimali kutoka Kenya ndugu Odenda Lumumba.

Mwanaharakati huyu mkongwe wa masuala ya ardhi na haki za binadamu katika ukanda huu wa Afrika Mashariki ni Mratibu wa kitaifa wa mtandao wa mashirika yanayotetea haki za ardhi nchini Kenya kwa zaidi ya miaka kumi sasa. Mtandao huu, pamoja na mambo mengine, ulishiriki kikamilifu katika mchakato wa kuandika Katiba mpya ya Kenya iliyozinduliwa rasmi mwaka 2010. Lumumba anaeleza namna walivyoshiriki, masuala waliyowasilisha kwa waandika Katiba pamoja na masuala ambayo hatimaye yalikubaliwa. Mtaalamu huyu wa sheria haishii hapo bali anachambua kwa undani changamoto walizokumbana nazo pamoja na namna walivyozikabili. Anaacha wosia kwa Watanzania kuwa, Katiba ndiyo maisha yenyewe kwa hiyo watu wanapaswa kutoacha mchakato huu uende bila wao kushiriki iwe kwa kuongea, kutembea au kushiriki kwenye mijadala mbalimbali rasmi na isiyo rasmi.

Kabla hata ya kuingia kwa undani kujua ni masuala gani waliyabeba, Lumumba anasema, mchakato wowote sharti uwe na wenyewe. Kwa upande wa Katiba, sharti la kwanza ni lazima wananchi waumiliki mchakato mzima wa utoaji maoni, ukusanyaji maoni na uchambuzi wa maoni ili zisichukuliwe tu hoja za wataalamu. Anasisitiza kuwa wamiliki wa mchakato wa Katiba ni wananchi. Hao ndio wenyewe.
Kuhusu ukusanyaji wa maoni ambayo ndiyo masuala muhimu ya kuingizwa kenye Katiba, inabidi kuhakikisha kuwa kila mwananchi na hasa makundi yanayosahaulika katika jamii yanapata nafasi ya kutoa mawazo yao kwenye fursa zao wenyewe bila kushurutishwa wala kulazimishwa kuamini wanacholetewa na wakubwa kutoka juu na hasa wanasiasa. Lumumba anasema Wakenya waliishi Katiba, maana walikuwa wakizungumza Katiba wakitembea Katiba, wakifanya kazi Katiba na hata kulala na ilipobidi, kuota Katiba. Kauli hii inamaanisha, kusiwe na vikwazo katika mjadala wa Katiba mpya kwa awaye yote wakati wowote na mahali popote.
Kwa upande wa masuala muhimu waliyokuwa wakishinikiza yaingizwe kwenye Katiba mpya ni pamoja na kupunguza mamlaka ya dola kwenye ardhi na kuyepeleka mamlaka hayo kwa wananchi wenyewe. Tofauti na zamani, ardhi nchini Kenya kwa sasa ni mali ya wananchi wala si dola tena.

Wakenya walihitaji pia kuwepo na mfumo wa usimamizi wa ardhi ulio wazi na unaotoa fursa sawa kwa wananchi kupata ardhi na kunufaika na ardhi ya taifa lao. Mfumo huu sharti uidhinishwe na bunge, lakini ni sharti uingizwe katika Katiba ili kuupa ulinzi zaidi dhidi ya wanasiasa ambao wamekuwa na kawaida ya kuhodhi ardhi dhidi ya raia wengine.

Pengine madai haya ndiyo ya msingi kuliko mengine yote maana moja ya sababu za wananchi wengi kukosa ardhi ni kwa vile mifumo mingi ya kiafrika imelimbikiza mamlaka za usimamizi na utendaji kwenye dola na vyombo vyake kiasi ambacho kadri wananchi wanavyokuwa mbali na mamlaka za kidola, ndivyo wanavyokosa nafasi ya kumiliki na kunufaika na ardhi ya nchi yao. Funzo kubwa kwa Watanzania ni kuwa makini katika kuchuja masuala ya kudai yaingizwe katika Katiba mpya na kuyasimamia kwa nguvu zote.

Kwa upande wa mbinu zilizotumika, Lumumba anasema kwanza walijenga mshikamano baina yao ili kuwa na sauti moja licha ya wingi wa makundi ya kijamii yaliyokuwa na madai kwenye Katiba mpya. Pili, wakatumia vyombo vya habari vya kila aina hasa redio za kijamii ambazo zilifikisha ujumbe hadi kwa njia ya lugha za makabila husika, tatu, kuchora ramani ya wazalishaji wadogo wadogo kwa kuzingatia mgawanyiko wao hasa wa wafugaji, wakulima, wavuvi wote kwa kuzingatia mahitaji ya kijinsia huku wakihusisha na madai yao. Nne, kuchuja maoni na kuyaweka katika maandishi kisha kuyasambaza kwa wananchi wote wayaunge mkono, na tano, kufanya mijadala na viongozi mbalimbali kwa lengo la kuwashawishi wakubali maoni ya wananchi. Jambo la muhimu kuliko yote, wananchi walihusika wao wenyewe kila hatua na kupeana mrejesho kila hatua iliyokuwa inapitiwa ili kutomuacha mwananchi yoyote nyuma na wala kuruhusu wapinzani wa vuguvugu kupandikiza hisia mbaya.
Kutokana na hayo yote, Katiba ya Kenya ilipoandikwa, zaidi ya asilimia 90 ya masuala yote yaliyopendekezwa na wananchi kuhusiana na ardhi yalikubaliwa. Ndani ya Katiba mpya ya Kenya, kuna sura nzima ya 5 inayoanzia ibara ya 60 hadi 68 ambayo inahusu masuala ya ardhi peke yake kuanzia misingi mikuu ya mfumo wa milki ya ardhi, vyombo vya usimamizi na taratibu za upatikanaji na udhibiti wa hakilimiliki. Katiba hiyo mpya haikuishia hapo, bali inatoa fursa ya kurejeshwa kwa ardhi ambayo ilichukuliwa hapo zamani kinyume na taratibu zilizokuwepo huku ikiwatambua na kuwawezesha kupata ardhi makundi ambayo yamekuwa yakinyanyasika kama vile wafugaji na wawindaji.

Yapo mengi ya kujifunza kutoka kwa Wakenya lakini pengine ni vema kusisitiza kuwa, kwa ulinganisho tu wa haraka mgawanyiko wa kijamii na hata kitabaka wa wakenya ni mkubwa sana kulinganisha na watanzania lakini waliacha tofauti zao kando wakapigania Katiba inayogusa maslahi yao wote katika utofauti wao. Watanzania tunapaswa kujifunza kukusanya nguvu za pamoja katika kupigania masuala yenye maslahi ya pamoja kama ilivyo kwa ardhi bila kukubali kutenganishwa na tofauti zetu mbalimbali.

Jambo la pili, dhamira ya kweli ya kuleta mabadiliko licha ya vikwazo ni muhimu sana. Wakenya walishakuwa wamejeruhiana sana wakati wa michakato ya uchaguzi na hata maandalizi ya Katiba mpya lakini hawakurudishwa nyuma na makovu ya tofauti zao hadi walipopata walichokihitaji. Hapa napo tuna jambo la kujifunza.

La tatu na muhimu zaidi ni mbinu zilizotumika. Kwa Wakenya, kila walichokifanya walijitahidi kukihusisha na Katiba mpya kuanzia sherehe za tohara na Ubatizo wa watoto hadi kwenye maziko na mazishi ya ndugu zao.

Watanzania tuna fursa lukuki za kuzungumza kwa uhuru na kuendeleza mdajala wa Katiba hadi itakapopatikana. Fursa hizo zipo kuanzia ngazi ya chini kabisa kwenye familia hadi juu kabisa kitaifa. Tuzitumie fursa hizo zote vizuri bila hofu ya kuzibwa midomo kwani kwa hilo, hata Katiba inayobadilishwa ilijitahidi kulinda uhuru wa maoni Katiba ibara yake ya 18 inayomruhusu kila mtu kuwa na uhuru wa maoni na kueleza fikra zake.

# Umuhimu wa Ardhi na Ulinzi

Inatoka uk. 3

wa kawaida hasa wanavijiji, ni kielelezo cha uhai wao, kielelezo cha utamaduni wao, kielelezo cha ubinadamu wao, pamoja na tegemeo lao la kuishi maisha ya kujitegemea na heshima".

Jambo la pili muhimu kuingizwa katika Katiba mpya ni Mfumo wa kumiliki ardhi unaozingatia usawa na haki. Hoja hiii inatokana na ukweli kuwa mfumo wa kumiliki ardhi uliopo nchini kwa sasa unalimbikiza mamlaka kubwa kwenye taasisi za serikali kuliko kwa wananchi. Pamoja na sheria kufafanua kuwa ardhi ni mali ya umma lakini maamuzi mengi kuhusiana na ardhi kama vile uwekezaji katika ardhi za vijiji yamekuwa yakifanywa na viongozi wa ngazi za juu. Endapo wanavijiji wangekuwa na sauti juu ya ardhi yao, basi wasingewekewa ukomo katika kugawa ekari 50 tu na zinazozidi hapo maamuzi yawe na vikwazo vya mamlaka za juu zisizohusika kabisa na ardhi ya kijiji. Katiba mpya lazima iainishe wazi mfumo wa Umiliki ardhi ambao utakuwa mikononi mwa wananchi na vyombo vyenye uwakilishi wa kutosha wa wananchi kama vile Bunge na Mikutano mikuu ya vijiji badala ya ilivyo sasa ambapo kamishina na wawakilishi wake katika wilaya na manispaa, wamepewa mamlaka kubwa juu ya ardhi wakati kimsingi wanaopaswa kuwa na sauti ni wamiliki na watumiaji wenyewe.

Shivji anafafanua zaidi na kusema, 'muundo wa udhibiti wa ardhi na taratibu za ugawaji wa ardhi ni masuala mengine muhimu ya kuingizwa katika Katiba mpya kutokana na kuwa uthibiti na ugawaji wa ardhi umekuwa unafanyika kiholela na kuacha wananchi wengi wakiwa hawana mahali pa kuishi na kulima. "Lazima wananchi wenyewe katika mjadala huu wa Katiba waainishe wanataka mfumo gani katika kudhibiti na kugawa ardhi kwa wenyeji na wageni maana kwa sasa kuna mifano hai katika Wilaya za Rufiji, Kilombero, Kilindi, Kisarawe na nyinginezo ya ugawanaji holela wa ardhi inayodhihirisha kuwa aidha hakuna udhibiti kabisa au mamlaka ya udhibiti imewekwa katika vyombo ambavyo sio makini" anasisitiza mjumbe huyu wa Baraza la Ushauri la Taasisi ya HAKIARDHI.

Msisitizo wa mwisho uliwekwa katika taratibu na kanuni za matumizi ya ardhi. Hapa hoja kubwa ikawa ni nani anayehusika kupanga matumizi ya ardhi? Kwa kutumia mifano ya uwekezaji katika sekta ya nishati mimea (biofuel) ni mwananchi gani angekuwa radhi kupanga ardhi iliyokuwa ikitumika au hata kama ni hazina kwa ajili ya uzalishaji wa chakula, itumike kulima mibono (jatropha? Ndiyo maana nchi kama Tanzania ambayo imejaliwa kuwa na rasilimali za kila namna inashangaza kulia njaa wakati kuna mashamba ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa chakula lakini mashamba hayo yanatumika kulima nishati uoto kunywesha magari ya Ulaya na Amerika.

*"ardhi kwa wananchi wa kawaida hasa wanavijiji, ni kielelezo cha uhai wao, kielelezo cha utamaduni wao, kielelezo cha ubinadamu wao, pamoja na tegemeo lao la kuishi maisha ya kujitegemea na heshima".*

Mfumo unazingatia usawa na haki kwa mujibu wa Profesa Shivji, hauna matabaka katika utoaji wa maamuzi na mgawanyo wa rasilimali za kitaifa kwani hakuna aliyechangia zaidi katika kuzifanya hizo rasilimali ziwepo. Sifa nyingine ya mfumo huu ni uwazi. Iweje basi mikataba inayohusu rasilimali za taifa iwe ni siri kati ya wanaozivuna na dola wakati wananchi ambao wamekuwa wakizilinda hawanufaiki nazo na wala hawapati nafasi ya kujua kilicho ndani ya mikataba hiyo. Mfumo wowote usio na misingi yake kwenye hisia, matakwa na matarajio ya watu, huishia kutoa tiba ya dalili za ugonjwa na kuuacha ugonjwa wenyewe kushamiri. Kwa mfumo uliopo, matatizo kama vile uporaji wa ardhi za wanavijiji unaofanywa na wasomi, wanasiasa na wawekezaji, upanukaji wa miji unaomeza vijiji, ukosefu wa uhakika wa chakula, ardhi ya uhakika ya malisho, kuibuka kwa makazi holela au yasiyo rasimi kwa lugha za watawala pamoja na kuendelea kusukumizwa pembezoni kwa jamii ndogo za wachimbaji, wavuvi na wakusanyaji matunda, kamwe hayawezi kutatuliwa yakaisha.

Pengine hitimisho la Profesa Shivji katika mada hii ndilo lenye kutia matumaini na pengine kutoa suluhu ya kudumu ya tatizo la kukosekana kwa uhakika wa milki ya ardhi kwa wananchi waishio ngazi ya msingi kabisa katika jamii. Kwa mtazamo wake, wananchi ni lazima watambue umuhimu wa Katiba katika maisha yao, na wamiliki mjadala na mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya inayozingatia maisha yao halisi. Wakiachiwa viongozi wa serikali, wanasiasa au taasisi za kiraia pekee kwa kisingizio kuwa wao ndio wenye utaalamu wa Katiba, watakuwa wameweka rehani maisha yao wenyewe. Jukumu la hayo makundi mengine yote ni kutoa jukwaa kwa wananchi kuelezea hisia zao na kuainisha namna wanavyotaka kuendesha maisha yao. Utaalamu una nafasi yake lakini si katika kusikiliza na kusikia mawazo ya wananchi na kuyageuza maana kama ilivyokwishazoeleka katika michakato mingine kwa kisingizio tu cha utaalamu. Bila shaka mawazo haya adhimu ndiyo chachu ya kuelekea kupata Katiba yenye mfumo wa milki, usimamizi na matumizi ya rasilimali uliojengwa katika misingi ya haki na usawa kwa Watanzania wote. Ni vema basi kujadiliana kwa hoja ili kutoacha hata chembe ya busara tunapoelekea kupata Katiba ya kihistoria kwa taifa letu katika kipindi cha miaka hamsini ya Uhuru.

Ardhi ni Uhai Januari - Aprili 2011

# Katiba bora itatokana na ushiriki mkamilifu wa Wananchi




Na Gloria Jimwaga

Wakati mchakato wa uandikaji Katiba mpya Tanzania ukiendelea katika hatua za awali, makundi mbalimbali yamekuwa yakiandaa mijadala inayotoa fursa kwa wananchi kutoa mawazo yao ya namna wanavyotaka Katiba mpya iwe na masuala ya kuyazingatia katika Katiba mpya. Wakati wa Kongamano la kujadili umuhimu wa ardhi na rasilimali za kitaifa kupewa ulinzi zaidi wa kikatiba ambalo liliandaliwa na taasisi ya HAKIARDHI hivi Karibuni, mwanaharakati wa masuala ya haki za kiuchumi na maisha endelevu kutoka shirika la Kimataifa la Oxfam, Marc Wegerif alitoa uzoefu wa uandikaji wa Katiba za nchi kadha wa kadha ikiwemo Afrika kusini na kusititiza kuwa, ulinzi wa rasilimali za taifa kama ardhi, madini, wanyamapori na misitu unategemea jinsi wananchi wanavyoshiriki kuweka misingi hiyo katika Katiba ya nchi.

Akitoa mfano wa nchi ya Afrika Kusini ambayo kihistoria ilikuwa katika mfumo wa utawala wa ubaguzi wa rangi, ndugu Marc alisema kuwa wananchi wengi hasa Waafrika walipata matatizo makubwa katika upatikanaji na umilikaji wa ardhi na rasilimali nyinginezo chini ya mfumo wa ubaguzi wa rangi lakini walipopata fursa ya kuandika upya Katiba yao, walihakikisha wanaweka misingi ya kukomesha uporaji mkubwa wa ardhi, madini na rasilimali nyinginezo uliokuwa ukifanywa na wazungu wachache dhidi ya raia weusi wengi. Haikuwa kazi rahisi kuweka misingi hiyo kwani iliwabidi kushawishi na ilipobidi kushinikiza kwa njia mbalimbali zaidi ya mazungumzo ya mezani kama vile maandamano, matembezi ya mshikamano, makongamano ya kitaifa na ya ngazi za chini kabisa, njia ambazo kwa pamoja zilifungua mlango wa kila mwananchi kutoa mawazo yake ambayo hatimaye yalichangia kuandikwa kwa Katiba waliyo nayo leo.

Kwa kutumia mfano wa mtaalamu huyu, kumbe inawezekana kubadili misingi ya mfumo wa milki na usimamizi wa rasilimali za taifa kwa njia za ushiriki mkamilifu wa wananchi. Hata hivyo, Marc anasisitiza kuwa haikuwa kazi rahisi kwani ilibidi kuwe na taasisi za wananchi wenyewe ambazo zilijitoa mhanga kuhakikisha kuwa misingi ya utu, usawa, haki na inayotoa fursa sawa kwa kila mwananchi inawekwa hata kwa gharama kubwa ya maisha yao kwani mfumo uliotangulia ulikuwa umewanyanyasa vya kutosha waafrika weusi katika nchi yao. Japokuwa Tanzania haiko katika mfumo wa ubaguzi




wa rangi wala ubaguzi mwingine wowote, vitendo vinavyoashiria mgawanyo usiozingatia haki na usawa katika umilikaji wa rasilimali ardhi na nyinginezo viko vingi kuanzia ngazi ya taifa hadi vijijini kwa wananchi wa kawaida. Pengine ni fursa yetu kama nchi kuchukua uzoefu huu wa Afrika Kusini taasisi na watu binafsi kuanza kufungua njia za mijadala ya kijamii ili wananchi wapate fursa ya kuchangia kuweka misingi katika Katiba yao. Taifa litapata maendeleo kutokana na wananchi wake kuwa na haki juu ya rasilimali zao na kuzitumia kujenga taifa lao. Fursa hiyo ya uhuru wa milki ya rasilimali sharti ijitokeze kuanzia kwenye sheria mama ya nchi ambayo ni Katiba.

Jambo la pili ambalo hata hivyo ndugu Marc alitahadharisha ni kuwa mabadiliko ya misingi ya kimfumo ni jambo moja lakini mabadiliko ya taratibu za uendeshaji na vitendo ambavyo vimejengeka kwa muda mrefu katika jamii ni jambo jingine na mabadiliko yake yanaweza kuchukua muda mrefu zaidi. Marc anatoa mfano kuwa licha ya kuwa Afrika Kusini walifanikiwa kupata Katiba mpya ambayo ilikuwa na mambo mengi yanayohusiana na haki za ardhi kwa wananchi wote, tabia, mienendo na taratibu za umiliki wa ardhi zinabadilika taratibu sana. Hadi sasa wananchi walio wengi hasa Waafrika weusi hawajarudishiwa maeneo ambayo yalitwaliwa ama kuporwa wakati wa ubaguzi wa rangi takribani wakulima 58,000 tu wa kizungu wakimiliki asilimia themanini (80%) ya mashamba makubwa ya kilimo.

Kama ilivyo katika jamii nyingine nyingi za kiafrika, wananchi wa kipato cha chini ndio wanaoishi katika maeneo yasiyopangwa kutokana na kuwa maeneo bora wanaishi watu wa tabaka la juu na wenye kipato cha juu hususan wafanyabiashara na wenye nafasi katika jamii. Katika hili, ni dhahiri kwamba wanawake na watoto ndio walioathirika zaidi na uporaji pamoja na mgao usiozingatia haki na usawa katika ardhi na rasilimali za taifa.



Hapa pia tunapata funzo kuwa uzuri wa Katiba na sheria uko katika utekelezaji wa yale yaliyo ndani yake. Lakini hata kama yamekuwa mazuri kiasi gani yasipopata nafasi ya kutekelezwa yakatoa manufaa kwa wahusika, basi uzuri wake hauna tija. Kwa kutumia mfano huo, bila shaka Watanzania watachukua tahadhari ya kutosha katika kuhakikisha kuwa Katiba na sheria mbalimbali hazibaki kuwa mapambo ya makabatini bali nyenzo muhimu katika kuwezesha upatokanaji wa haki za wananchi. Ili kufikia hatua hiyo, nafasi ya wananchi hususan kupitia vikundi vyao na watu binafsi ni muhimu kushinikiza utekelezaji wa vifungu husika kwa njia mbalimbali maana haki iliyo katika Katiba au sheria isipotekelezwa si haki.

Licha ya mada ya ndugu Marc kuwasisimua washiriki wengi kwa namna alivyokuwa akigusia masuala yenye hisia kutoka mfumo wa kibaguzi, tahadhari ilitolewa kuwa mabadiliko ya Katiba si lelemama bali ni jambo linalokabiliwa na changamoto nyingi. Alizitaja baadhi ya changamoto kuwa ni pamoja na uadui na uhasama kutoka kwa wasiotaka kubadilika hasa kutokana na kunufaika na mfumo uliopo, kununuliwa kwa baadhi ya viongozi wa mabadiliko na matumizi ya fedha aghalabu kutokana na uhaba wa rasilimali kwa wanaoshiriki mchakato wa mabadiliko. Akifafanua, Marc anasema, wanaotaka mabadiliko ya kimfumo mara nyingi ni watu walio nje ya mfumo, wale wasionufaika na kinachoendelea na wale ambao wamewekwa pembezoni. Hawa kwa hapa kwetu ni wakulima, wafugaji, wavuvi, wakusanya matunda, wachimbaji wadogo na jamii za namna hiyo. Kwa namna mifumo yao ya utafutaji riziki ilivyo, watu hao ni rahisi kununuliwa na hata kulaghaiwa na wenye nacho kwa kisingizio cha kuwakilishwa au kusaidiwa.

Marc anashauri kuwa ili vuguvugu la mabadiliko liwe endelevu ni sharti kuwa na safu zaidi ya moja za uongozi wa kijamii. Hii itasaidia pale ambapo safu moja imenunuliwa safu nyingine kuendelea na uongozi wa vuguvugu bila kifisha harakati. Uzoefu wa Afrika Kusini unaonyesha kuwa wananchi walijipanga katika nafasi zao sawa sawa wakahimili mateso na ghiliba za wabaguzi waliokuwa wakitumia vibaraka kusaliti jitihada za mabadiliko hadi pale walipofanikiwa kuweka misingi ya mfumo mpya uliopo sasa.

Mada hii ilitoa mafunzo mengi sana kwa washiriki lakini zaidi ya yote ni namna ambavyo wananchi wakishiriki kikamilifu katika mchakato wa mabadiliko wanavyoweza kuleta mabadiliko ya kweli yanayozingatia utu wao, usawa, uzalendo na mahitaji yao kutokana na rasilimali zao. Ni jukumu basi la asasi kama hakiardhi kuendelea kuchochea vuguvugu hili ili moto walioondoka nao wananchi katika kongamano hili usizimike hadi pale Katiba mpya itakapopatikana.



*Wananchi wakichambua mswaada wa Katiba nje ya ukumbi wa Bunge, Dodoma.*



Na Saad Ayoub

# Na huu ndio wajibu wa NGOs katika mchakato wa Katiba mpya



Na Deus Kibamba

Ni katika ukumbi wa Landmark hapa hapa Ubungo na ni siku ya pili ambayo wananchi wanaendelea na mjadala wa jinsi ambavyo ardhi na rasilimali za taifa zinavyopaswa kuwa nguzo muhimu ya Katiba mpya. Deus Kibamba ndiye anayechokoza mjadala na anaanza kwa kuuliza swali kwa washiriki "je tumejipangaje kuekea kupata Katiba mpya? Hatuwezi kujipanga kama hatujijui sawasawa sisi ni akina nani na madai yetu katika Katiba ni yapi"

Anatanabaisha kuwa, wajibu wake ni kuwafanya watu wajitambue na kubeba majukumu yao katika mchakato wa mabadiliko makubwa ya kimfumo kwa njia ya kuleta Katiba mpya. Ili washiriki waone umuhimu wa kujitambua na kubeba majukumu yao ipasavyo, Ndugu Kibamba anatoa historia ya uundwaji wa Katiba katika Tanzania tangu uhuru 1961, kisha 1962, 1965, 1977 na hatimaye wakati wa marekebisho yote 14 yaliyofanywa kwenye Katiba ya 1977 tuliyo nayo sasa. Anasema miongoni mwa mapungufu ya Katiba hizo hasa ile ya mwaka 1965 ni kuua misingi mikuu ya demokrasia kama vile nafasi ya mgombea binafsi, uwepo wa vyama vingi pamoja, uwepo wa taasisi za kiraia na uhuru wa kutosha wa vyombo vya habari na kusisitiza kuwa "Kwa sasa Watanzania inabidi tubadilishe mambo kutoka katika mazoea kwenda katika uelekeo wenye lengo la kuimarisha maisha na uwezo wa nchi kujiamulia mambo yake yenyewe pasipo kuingiliwa na mafedhuli."

Watu wanahamasika wanataka kuchangia hasa baada ya kubaini kuwa kumbe hawakushiriki kikamilifu katika kuandaa Katiba zilizopita na yalikuwa makosa ya serikali lakini anawaambia, tulieni kwanza huenda nikimaliza mada mtajitambua kuwa yalikuwa makosa yenu pia, kisha mtachagua kuendelea kurudia makosa au kujirekebisha.

Wengi wa washiriki hawa wanatoka kwenye asasi za kiraia maarufu kama NGOs na Ndugu Kibamba anatumia muda huu kuwakumbusha wajibu wao. Anaanza kwa kusema, wana asasi si kama watu wengine katika jamii maana wao wameshapiga hatua kadhaa mbele na kufikia mahali wakajisahau wakadhani wao ndio watu bora zaidi ya wengine. Sio tu katika maendeleo yao binafsi kwa vile wanapata mshahara wa kazi wanazofanya laini, pia kwa maarifa na taarifa maana wana asasi wengi wamesomeshwa kwa hela za walipa kodi na wanashahada hadi za ngazi ya juu kabisa. Kwa kuwa wana taarifa na maarifa, jukumu lao kubwa ni kuhakikisha wanakuwa chachu ya mabadiliko ya Katiba katika nchi hii bila kujivika joho la wananchi wote.


Kwa mujibu wa Ndugu Kibamba, ili mabadiliko ya Katiba yatokee, mambo matano muhimu yanapaswa kuzingatiwa kwa pamoja kati ya wananchi na NGOs. Kwanza, sharti kuwe na dhamira ya kuleta mabadiliko bila kujali yatokanayo na dhamira hiyo yawe mazuri au mabaya. Watu wengi wana hofu kuwa mabadiliko ya Katiba yanaweza kuleta matokeo yasiyo mazuri hasa kwa kuipunguzia mamlaka dola juu ya haki na uhuru wa raia. Hata hivyo, hisia kama hizi zikiruhusiwa, wananchi wataacha fursa ya kunufaika na mema yanayotarajiwa kuletwa na Katiba mpya na mifumo yake. Dhamira ni nia au msukumo wa dhati kabisa wa ndani ya mtu. Kila raia akiwa na msukumo huu, mchakato wa Katiba mpya unaweza kuwa mfupi kuliko inavyotarajiwa. Kibamba anaweka msisitizo kuwa, wajibu wa asasi za Kiraia ni kuhakikisha dhamira hii inakuwepo katikati ya makundi ya watu wenye mitizamo tofauti hata hao wasio na tumaini la mabadiliko. Hapa panahitaji hamasa ili kuamsha hiyo dhamira na ari ya kushiriki kuleta mabadiliko.

Pili, asasi zina wajibu wa kufanya uchambuzi yakinifu wa kuhusisha maisha ya kila siku ya mwananchi na fursa ya Katiba mpya kuyaboresha ili mchakato wa Katiba ujikite katika hisia na hali halisi ya maisha pia. Uchambuzi huu unapaswa utokane na tafiti katika maeneo mbalimbali pamoja na uzoefu uliojengwa katika taarifa zilizokusanywa kwa njia za utafiti na njia nyinginezo pia. Uchambuzi huu, ukisambazwa kwa upana kwa njia za vyombo vya habari, vuguvugu la madai ya Katiba litakuwa na wigo mpana zaidi na kuwezesha mchakato kumilikiwa na wananchi wote

Kazi kubwa ya tatu ya asasi za kiraia ni kuondoa fikra mgando za walio katika madaraka za kutotaka kubadilika kwa vile ama wananufaika na mifumo iliyopo au wana hofu kuwa mabadiliko yakitokea yatatoa fursa ya kuwajibishwa kwa maamuzi na matendo yao mabaya kama vile ubadhirifu na matumizi mabaya ya rasilimali za taifa. Fikra hizi mgando zitaondolewa kwa harakati za ushinikizaji, ushawishi na utetezi wa hoja. Katika jukumu hili Ndugu Kibamba anaonya kuwa

Endelea Uk.9

*Inatoka uk. 8* ni sharti asasi zijichimbie kutafuta taarifa za kutosha na vielelezo vya kuthibitisha hoja ili madai yasibezwe na wasiotaka mabadiliko kwa urahisi.




*Wananchi wamedhamiria kuleta mabadiliko na wako tayari kuhamasisha wanajamii wenzao*

Jambo la nne muhimu kwa mujibu wa Ndugu Kibamba ni kutambua kikwazo kikubwa kuliko vyote cha mabadiliko yanayokusudiwa ambacho ni watu wasiojali kinachoendelea. Hawa ni raia wengi wasiotaka kutimiza wajibu wao na ambao kutokujali kwao kunatokana na kukata tamaa. Hawajitokezi kupiga kura, hawalipi kodi, hawahoji wala kudhihirisha kwa vitendo kuwa wamekereka na maovu kila yanapojitokeza, na hawajitolei kufanya shughuli za maendeleo. Kwa ujumla, wamelala fofofo. Ni jukumu letu kuwaamsha na kuwafanya waone ipo haja ya kuwa hai. Kama NGOs ni chachu ya mabadiliko, basi wanapaswa "kuwachachusha" na kundi hili liwe sehemu ya mchakato wa Katiba mpya.

Na tano, asasi zina wajibu wa kutambua kuwa malengo ya mabadiliko yanapaswa kuwa endelevu na hasa yajikite katika kuleta mabadiliko ya kimfumo ya muda mrefu badala ya kutatua matatizo ya wakati huu tu. Kesho yetu inategemea sana leo yetu. Hata hivyo anaonya kuwa ikiwa mchakato utachukua muda mrefu unaweza kupoteza maana na malengo na kuwapa upenyo wale wanaopinga mchakato huo kuchukua nafasi ya kuvuruga na kukwamisha malengo ya Katiba mpya na badala yake ikawa Katiba bomu kuliko hiyo iliyopo.

Hamasa iliyojitokeza baada ya mada hii ya Ndugu Kibamba ilikuwa ishara tosha kuwa wananchi wamedhamiria kuleta mabadiliko na wako tayari kuhamasisha wanajamii wenzao katika mchakato huu wa uandikaji Katiba mpya. Changamoto kubwa ikawa nani aongoze harakati hizi? Matumaini yalipatikana baada ya washiriki kujulishwa kuwa Kituo cha Taarifa kwa wananchi yaani (Tanzania Citizens Information Bureau-TCIB) kinaratibu mchakato wa uandikaji Katiba mpya kupitia JUKWAA LA KATIBA ambao ni mtandao wa mashirika na wananchi waliojiunga pamoja kwa kujitolea kuwa na jukwaa la kuzungumzia na kutolea mawazo yao.

Baada ya kujibu hoja nyingi za wachangiaji, Ndugu Kibamba anahitimisha kwa kutoa wito wa asasi za kiraia, kutochukua nafasi ya wananchi bali kutoa fursa kwa kila raia kutoa mawazo yake. Kwa mawazo yaliyoonekana kukubaliwa na wengi anasema, "katika kipindi hiki kutakuwa na watu mbalimbali kupitia majukwaa yao wakipaza sauti zao za kutaka madai yao yasikilizwe ikiwa ni pamoja na majukwaa ya ardhi, wanawake, walemavu, wanaoishi na virusi vya Ukimwi, wavuvi, wafanyakazi na wakulima. Kila mwananchi anatakiwa kutoka huko msituni alikojificha na kuja kutoa maoni yake katika jukwaa linalomuhusu na baadaye jumuiko la majukwaa yote kupaza sauti moja kama taifa kuhusu kile wananchi wanachokitaka katika Katiba yao". Watu hawa wanahitaji kuratibiwa kuhimizwa, kuhamasishwa, kuwezeshwa, kutiwa moyo, kuvumiliwa na kufunguliwa fursa za kushiriki kikamilifu kwenye mchakato ili mawazo yao yawe sehemu ya Katiba na mfumo mpya wa utawala wa nchi. Wajibu wa kufanya hayo yote na mengine yasiyotajwa ni wa NGOs katika mchakato wa kuelekea kupata Katiba mpya.

# Mawazo ya Wananchi kuhusu Katiba mpya ya Tanzania

Washiriki wa mjadala wa kitaifa juu ya umuhimu wa kuingiza suala la ardhi na rasilimali za kitaifa katika Katiba mpya lililofanyika kwenye ukumbi wa hoteli ya Landmark iliyoko Ubungo jijini Dar es salaam walipata fursa ya kuchangia katika mjadala huu wa siku mbili kuanzia tarehe 25-26 Februari 2011 na haya ndiyo waliyosikika wakiyasema.



**Prof. Aida Isinika- Mhadhiri –SUA-Morogoro.** *Tujenge kwanza maadili ya taifa*

Tokea uhuru wa Tanganyika ni awamu moja tu ya uongozi iliyozingatia maadili lakini baaada ya hapo kumekuwepo na mmomonyoko mkubwa sana wa maadili kwa wananchi na viongozi, wasomi na wasiokuwa wasomi. "Mimi naamini kwanza tunapaswa kurejesha maadili ya uongozi na maadili ya umma na hapa ndipo hata hiyo Katiba mpya itakuwa na tija lakini bila maadili Katiba haitasaidia. Tunahitaji kubadilika sana kimaadili ili tuweze kuleta mabadiliko katika usimamizi wa rasilimali,"



**Ally Abbas Yusuph - Mkulima –Rufiji.** *Tusiwaburuze wananchi wa vijijini*

Wanavijiji wana uelewa sana wa mambo yao zaidi hata ya watu wa mjini. Matatizo tuliyo nayo yanatokana na viongozi ambao tunawaita wasomi na wanaishi mijini. Mimi nina uzoefu mkubwa sana na wananchi hawa kwa jinsi walivyoshiriki katika harakati za masuala ya rasilimali na ardhi kwa muda mrefu tu na wakafanikiwa kuikomboa hata hiyo Delta ya Rufiji. Ninyi NGOs na Wanasiasa mnapaswa kuwafikia wananchi katika mchakato huu wa Katiba mpya na kupata mawazo yao kule waliko siyo kukaa maofisini na kujifungia mkijifanya wataalamu. Wao ndio hasa wenye utaalamu, wapeni fursa muone na kusikia watakayoyasema.

**Baraka Saiteu – CELG – Dar es Salaam.** *Tuwe na kauli moja ya jukwaa la Katiba*

Kutumia majukwaa mbalimbali kama vile jukwaa la ardhi, la jinsia, la afya n.k, katika mchakato wa Katiba mpya ni mfumo mzuri kwa jinsi yanavyowakilisha matakwa ya wahusika wenyewe wa majukuwaa hayo. Hata hivyo, angalizo langu ni kwenye utaratibu wa kuyaratibu haya majukwaa ili yaweze kuwa na kauli moja wakati wa kupeleka madai yao ya kuingizwa kwenye Katiba mpya.Yakipishana lugha, lazima serikali itatumia udhaifu huo kutowashirikisha.

**Salma Twahir – Mkulima Kigamboni.** *Tuunde kamati ndogondogo*

Naunga mkono hoja ya Alli Abbas Yussuf kuwatumia wanavijiji zaidi katika mchakato wa Katiba mpya kuliko watu wa mijini kwa kuwa watu wa mijini ni rahisi kurubuniwa na kuwasaliti wanavijiji ambao ndio wengi. Nasema hivyo kwakuwa nina uzoefu na yanayotukumba kule Kigamboni na jinsi tulivyoweza kuyashughulikia sisi kama wananchi kwa kutumia kamati zetu ndogondogo.



**Abdallah Matata - Buyuni Chanika.** *Tujipangie muda wa kuwa na Katiba mpya*

Ni lazima kuwe na muda maalum wa kukamilisha mchakato huu wa kudai Katiba mpya ili tusiende bila kuwa na ratiba wala picha kamili ya mabadiliko yatakuwa lini. Kwa kweli uchaguzi ujao lazima ufanyike chini ya Katiba mpya.

**Dinno Celestin - Cords – Kiteto.** *Haki ya ardhi kwa mfugaji iwe pia ya kikatiba*

Kwa jinsi ambavyo wafugaji tumesaulika na kuachwa kutangatanga kama yatima ndani ya nchi yetu wenyewe, ni lazima hiyo Katiba mpya ije mapema kutuoondolea utumwa huu. Tunataka Katiba itamke wazi kuwa sisi ni raia wa Tanzania wala si Wakenya na kwamba tuna haki ya kumiliki ardhi na kuchunga mifugo kama ambavyo wakulima na wawekezaji wananufaika nayo.

# KONA YA UFAHAMU

### Katiba maana yake ni nini?

Ni muongozo wa kisheria ambao huainisha muundo na shughuli za mihimili ya dola katika taifa na kuchanganua mipaka ya kimamlaka, haki, wajibu na mahusiano kati ya wananchi na dola na baina ya vyombo mbalimbali. Katiba katika nchi ndiyo sheria mama kwa misingi kuwa, sheria zote zinazotungwa sharti ziendane na misnigi ya kiKatiba isiwepo sheria inayokinzana na Katiba.

### Sheria ni nini?

Sheria ni nyenzo (amri, mfumo, taratibu, masharti) ya kimamlaka ya kutekeleza au kukidhi matakwa ya kimaamuzi na makusudio yaliyo katika Katiba au sera. Sheria hutoa tafsiri ya haki, wajibu na makusudio yaliyoelekezwa kwenye Katiba au sera kuhusiana na jambo au sekta husika. Bunge ndilo lenye mamlaka ya kutunga sheria. Hata hivyo, ili sheria ianze kufanya kazi ni sharti iridhiwe na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Baada ya kuridhiwa, waziri mwenye dhamana husika ni sharti atangaze kwenye gazeti la serikali kuanza kutumika kwake.

### Kanuni ni nini?

Kanuni ni sheria ndogo zinazotungwa na mamlaka mbalimbali kwa idhini ya bunge ili kuwezesha utekelezaji wa sheria husika. Mara nyingi, mawaziri wamepewa mamlaka ya kutunga kanuni za sheria zilizo katika wizara zao. Kwa mfano, kanuni za Sheria ya Ardhi namba 4 na Sheria ya Ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999 zilitungwa mwaka 2002.

### Sera ni nini?

Sera ni mwongozo au dira inayobeba matamko yenye dhamira ya kutoa msukumo katika ufanikishaji wa jambo hasa la kisekta. Kwa kawaida, matamko hayo ya kisera hutekelezwa na sheria katika sekta husika. Sera siyo sheria na wala mtu hahukumiwi kwa kukiuka sera bali sheria, ingawa yale yaliyokiukwa katika sheria yanaweza kuwa ni maagizo ya sera.



*Mjadala wa Katiba si lazima ufanyike ukumbini kama wanavyodhihirisha wananchi hawa.*

# Mawazo ya Wananchi

*Inatoka uk. 9*

**Angela Mwageni - MPLC.** *Katiba mpya idhibiti wawekezaji wanaopora rasilimali za taifa*

Tumeshuhudia wawekezaji wakipora ardhi kwa kushirikiana na Watendaji wa Vijiji na wa Halmashauri za Wilaya wasiyo waadilifu. Katiba mpya izuie mianya kama hiyo maana sheria kama zipo zimeshindwa na pia wale wote waliohusika na uporaji wa ardhi hasa za wananchi Katiba iwe na mfumo wa kuwawajibisha ikiwemo kurudisha ardhi waliyopora na kugawiwa kwa wananchi.



**Martha Laurent Sumaye – Mfugaji-Manyara.** *Katiba irejeshe utu kwa wananchi wazalendo*

Kwani sisi tunaonekana watu basi? Siku hizi hata utu wetu umechukuliwa na wenye fedha. Kama Katiba hii itasaidia kuturejeshea utu wetu sawa lakini kama tutaendelea kunyanyaswa na wageni hasa kama wale wa kule Hanang, basi hamna hata sababu ya kuwa nayo.

HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI



*Makazi ya Mwananchi pembezoni mwa Mgodi*

Anuani/Ofisi
Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**, Kitalu Na. 236 Sinza Mori
S.L.P. 75885, DSM, Tanzania. Simu +255 22 2771360 /Faxi +255 22 2771362, +255 784 646 752.
Baruapepe: info@hakiardhi.org Tovuti: www.hakiardhi.org

## MACHAPISHO

| Na. | Jina la Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|
| 1. | Ripoti ya Tume ya Rais kuhusu maswala ya Ardhi - *1994* | Wizara ya Ardhi |
| 2. | Ardhi ni Uhai - *1995* | Georgios Hadjivayanis |
| 3. | Not Yet Democracy: *Reform land tenure in Tanzania - 1998* | Issa G. Shivji |
| 4. | Haki za Wamaasai waishio Hifadhi ya Ngorongoro *1999* | Issa G. Shivji, Wilbert Kapinga |
| 5. | Mwongozo wa Haki za Ardhi kwa Wananchi wa Tanzania - *2002* | Issa G. Shivji/ Deus Kibamba |
| 6. | Fukuto la Migogoro ya Maeneo na Hatma ya Wazalishaji Wadogo Wadogo Tanzania - *2002* | Aida Isinika |
| 7. | The Silences in the NGO Discourse - Occasional Paper No. 1 - May, *2006* | Issa G. Shivji |
| 8. | The Mute Plunder 'Bioresources & dispossession in Tanzania 2008 | Ng'wanza Kamata |
| 9. | Public Perceptions on Bio Resources Conservation in Tanzania Occasional Paper No. 2 - Julai, *2008* | Issa G. Shivji |
| 10. | Accumulation by Land dispossession and Labour Devaluation in Tanzania 2011 | Hakiardhi |
| 11. | Maswali na Majibu yanayohusu mfumo wa milki na usimamizi wa ardhi nchini "Kitini cha Kujielimisha" 2011 | Hakiardhi |
| 12. | Muongozo wa mafunzo juu ya sheria za ardhi na utawala katika muundo wa Serikali za mitaa 2011 | Hakiardhi |